HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 29/04/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU.

Wajumbe waliohudhuria:

1.	Mhe. Pascal M. Kihanga	__	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Ndg. Sheilla E. Lukuba	__	Mkurugenzi wa Manispaa – Katibu
3.	Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele	__	Naibu Meya
4.	Mhe. Latifa Saidi Ganzel	__	Mjumbe
5.	Mhe. Namala Johaness Mchunguzi	__	Mjumbe
6.	Mhe. Warda Omari Bazia	__	Mjumbe
7.	Mhe. Marco Mathias Kanga	__	Mjumbe
8.	Mhe. Melchior Peter Mwamnyanyi	__	Mjumbe
9.	Mhe. Rahma Lashayo Maumba	__	Mjumbe
10.	Mhe. Mwanaidi Ebrahim Ngulungu	__	Mjumbe
11.	Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu	__	Mjumbe
12.	Mhe. Abdallah Ally Meya	__	Mjumbe
13.	Mhe. Selestini Savini Mbilinyi	__	Mjumbe
14.	Mhe. Hadija Kombo Kibati	__	Mjumbe
15.	Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	__	Mjumbe
16.	Mhe. Juma Issa Kiduka	__	Mjumbe
17.	Mhe. Salum Mrisho Chunga	__	Mjumbe
18.	Mhe. Zuberi George Mkalaboko	__	Mjumbe
19.	Mhe. Samuel Alfred Msuya	__	Mjumbe
20.	Mhe. Hamisi Ally Kilongo	__	Mjumbe
21.	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	__	Mjumbe
22.	Mhe. Mch. Thomas Benedict Butabile	__	Mjumbe
23.	Mhe. Amina Hussein Zihuye	__	Mjumbe
24.	Mhe. Rashid Ramadhani Matessa	__	Mjumbe
25.	Mhe. Amini Abdallah Tunda	__	Mjumbe
26.	Mhe. Eng. Hamisi Hamadi Ndwata	__	Mjumbe
27.	Mhe. Aisha Ahmad Kitime	__	Mjumbe
28.	Mhe. Emmy Kiula Rajabu	__	Mjumbe
29.	Mhe. Grace Luwis Mkumbae	__	Mjumbe
30.	Mhe. Zinduna Kombo Selemani	__	Mjumbe
31.	Mhe. Lt.Col(Mst) Ahmed S. Mazora	__	Mjumbe
32.	Mhe. Salima Bonzo Mbandu	__	Mjumbe
33.	Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu	__	Mjumbe
34.	Mhe. Joel Albert Kisome	__	Mjumbe
35.	Mhe. Seif Zahoro Chomoka	__	Mjumbe

36.	Mhe. Madaraka Steven Bidyanguze	__	Mjumbe
37.	Mhe. Athumani Omary Lujuo	__	Mjumbe
38.	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	__	Mjumbe
39.	Mhe. Hassan Madadi Maringo	__	Mjumbe
40.	Mhe. Peter Joel Dhahabu	__	Mjumbe

Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa

1.	Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood (Mb)	__	Mjumbe
2.	Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma (Mb)	__	Mjumbe
3.	Mhe. Norah Mzeru (Mb)	__	Mjumbe

Waalikwa waliohudhuria

1.	Mhe. Bakari Msulwa	__	Mkuu wa Wilaya ya Morogoro
2.	Mhe. Highness L. Munisi	__	Katibu wa CCM Wilaya
3.	Mhe. Fikiri H. Juma	__	Mwenyekiti wa CCM Wilaya
4.	Ndg. Francis G. Francis	__	Kaimu Katibu Tawala Mkoa
5.	Ndg. Hilary B. Sagara	__	Kaimu Katibu Tawala Wilaya
6.	Ndg. Lusajo Kamendu	__	Afisa Usalama
7.	Mhe. Maulidi Chambilila	__	Katibu Mwenezi na Siasa CCM Wilaya
8.	Eng. Bertam B. Minde	__	Kutoka MORUWASA
9.	Eng. Erick Mtambi	__	Kutoka TARURA Manispaa

Wakuu wa Idara na Vitengo waliohudhuria;

1.	Ndg. Pilly R. Kitwana	__	Afisa Utumishi wa Manispaa
2.	Ndg. Neema Michael Dachi	__	Mkaguzi wa ndani wa Manispaa
3.	Ndg. Jeremiah Lubeleje	__	Mchumi wa Manispaa
4.	Dr. Ikaji Z. Rashid	__	Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa
5.	Ndg. Samwel Subi	__	Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Manispaa
6.	Ndg. Jafari A. Makupula	__	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi wa Manispaa
7.	Ndg. Safia Kingwahi	__	Afisa Utamaduni wa Manispaa
8.	Ndg. Shabani Duru	__	Afisa Usafirishaji wa Manispaa
9.	Ndg. Amina Kireti	__	Kaimu Katibu TSC Manispaa
10.	Ndg. Epiphania Matafu	__	Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
11.	Ndg. Stephen N. Mkulia	__	Kaimu Afisa Elimu Msingi wa Manispaa
12.	Ndg. Enedy Mwanakatwe	__	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa
13.	Ndg. Elikarim Tyeah	__	Kaimu Mwanasheria wa Manispaa
14.	Ndg. Nesphora Kinoge	__	Kaimu Mratibu wa kudhibiti UKIMWI Manispaa
15.	Ndg. Pendo Chagu	__	Afisa Uchaguzi wa Manispaa
16.	Dr. Tito Kagize	__	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Mansipaa

17.	Eng. Juma Gwisu	__	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa
18.	CPA. Edward B. Malima	__	Mweka Hazina wa Manispaa
19.	Ndg. Kitutu Mshana	__	Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa
20.	Ndg. Festus Herman	__	Afisa Biashara wa Manispaa
21.	Ndg. A. Mwakipesile	__	Kaimu Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
22.	Ndg. Ruben E. Urassa	__	Mchumi
23.	Ndg. Nancy Fletcher	__	Kaimu Mratibu wa TASAF Manispaa

Watendaji wa Kata waliohudhuria

1.	Ndg. Mariamu S. Rajabu	__	Mtendaji wa Kata ya Mbuyuni
2.	Ndg. Asha H. Muvogogo	__	Mtendaji wa Kata ya Mafiga
3.	Ndg. Helen W. Mgallah	__	Mtendaji wa Kata ya Bigwa
4.	Ndg. Pato Haule	__	Mtendaji wa Kata ya Sultani Area
5.	Ndg. Michael Mgowe	__	Mtendaji wa Kata ya Lukobe
6.	Ndg. Laurent Masanja	__	Mtendaji wa Kata ya Mkundi
7.	Ndg. Baraka Lemaha	__	Mtendaji wa Kata ya Mindu
8.	Ndg. Evance Y. Kutona	__	Mtendaji wa Kata ya Kichangani
9.	Ndg. Edwin A. Song'ora	__	Mtendaji wa Kata ya Mazimbu
10.	Ndg. Rajabu Wanyamale	__	Mtendaji wa Kata ya Chamwino
11.	Ndg. Ibrahim S. Kobby	__	Mtendaji wa Kata ya Mafiga
12.	Ndg. Sikudhani Jasson	__	Mtendaji wa Kata ya Tungi
13.	Ndg. Jeniffer S. Rashid	__	Mtendaji wa Kata ya Kauzeni
14.	Ndg. Ibrahimu R. Nguya	__	Mtendaji wa Kata ya Kingolwira
15.	Ndg. Esther Kulwa	__	Mtendaji wa Kata ya Kingo
16.	Ndg. Patricia Sichome	__	Mtendaji wa Kata ya Mji Mkuu
17.	Ndg. Prisca Mawallah	__	Mtendaji wa Kata ya Mzinga
18.	Ndg. Shani A. Sudi	__	Mtendaji wa Kata ya Kihonda Maghorofani
19.	Ndg. Bright Sospeter	__	Mtendaji wa Kata ya Kilakala
20.	Ndg. Abuu R. Liwangila	__	Mtendaji wa Kata ya Mafisa
21.	Ndg. Amina Saidi	__	Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo
22.	Ndg. John Joseph	__	Mtendaji wa Kata ya Luhungo
23.	Ndg. Tausi Z. Athumani	__	Mtendaji wa Kata ya Magadu
24.	Ndg. Aziza Omari	__	Mtendaji wa Kata Kiwanja cha Ndege
25.	Ndg. Tatu H. Ally	__	Mtendaji wa Kata ya Kihonda
26.	Ndg. Fatuma Mkwenda	__	Mtendaji wa Kata ya Sabasaba
27.	Ndg. Anna J. Swai	__	Mtendaji wa Kata ya Mji Mpya

28.	Ndg. Martha N. Kipanga	__	Mtendaji wa Kata ya Uwanja wa Taifa
29.	Ndg. Hamisi A. Ismail	__	Mtendaji wa Kata ya Boma

Sekretarieti:-

1.	Ndg. Daudi A. Kibwana	__	Katibu wa Mikutano
2.	Ndg. Deogratias Butabile	__	Katibu wa Mikutano
3.	Ndg. Sylvia Kahitwa	__	Katibu wa Mikutano
4.	Ndg. Theresia Mbena	__	Katibu wa Mikutano
5.	Ndg. Lilian Henerico	__	Afisa Habari

HMM/BM/30/ 2020/2021 Kufungua Mkutano

Kabla ya kufungua Mkutano, uliimbwa wimbo wa Taifa na Dua ya kuiombea Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Baada ya Dua Mkurugenzi wa Manispaa aliwatambulisha Wajumbe na Wageni waalikwa.

Mstahiki Meya (Mwenyekiti) aliwakaribisha Wajumbe na Wageni waalikwa kwenye Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani na alifungua Mkutano saa 5:10 Asubuhi.

Baada ya kufungua Mkutano Mstahiki Meya aliwakaribisha Viongozi mbalimbali ili waongee na Madiwani, Watendaji na Wananchi kama ifuatavyo:-

1.0 Inspector wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Morogoro

Alieleza kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kuadhimisha wiki ya maonesho ya Zimamoto na Uokoaji Kitaifa yatakayofanyika Mkoa wa Morogoro kuanzia tarehe 17/5/2021 katika kiwanja cha Tumbaku.

Ombi

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliomba Waheshimiwa Madiwani wasaidie kuwezesha ufanikishaji wa maadhimisho hayo. Aidha, ilielezwa kuwa kutakuwa na michezo mbalimbali kama vile Mpira wa Miguu, Netball na Vollyball kwa muda wa siku tano. Mstahiki Meya pamoja na Madiwani waliombwa wawepo siku ya uzinduzi tarehe 17/5/2021 na siku ya kilele tarehe 21/5/2021.

Inspector wa Jeshi la Zimamoto alieleza kuwa bajeti yao ni finyu hivyo wanahitaji maji na fedha kutoka kwa Wadau na Halmashauri.

Mstahiki Meya alipokea ombi hilo na alimuelekeza Inspecter wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Morogoro kuandika barua ya maombi kwa Mkurugenzi wa Manispaa.

2.0 Salamu za Katibu wa CCM Wilaya.

Mheshimiwa Highness L. Munis Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya aliehamia Manispaa ya Morogoro kutoka Mkoa wa Manyara alijitambulisha na kuwasalimia Madiwani na Watendaji na kuomba kupewa ushirikiano.

Baraza lilipokea taarifa hiyo.

3.0 Salamu za Mwenyekiti wa CCM Wilaya.

Alieleza kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilitembelea Bwawa la Mindu mwezi Machi, 2021 Kamati hiyo ilihoji Idara ya Kilimo ya Manispaa ya Morogoro inashughulika vipi kuendeleza Kilimo kwenye maeneo yanayozunguka bwawa hilo kama vile eneo la Mindu hadi Kingolwira.

Kuhusu uvunaji wa rasilimali ya samaki.

Aliomba Halmashauri ipange utaratibu mzuri wa uvuaji wa samaki katika Bwawa la Mindu.

Kuhusu upelekaji wa fedha za maendeleo kwenye Kata.

Aliipongeza Halmashauri kwa kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Kata kwa ajili ya miradi ya Jamii, Maji na Elimu.

Aliomba kila kikao cha Kamati kiwe kinajadili agenda ya kuongeza ajira za vijana kama vile Viwanda, kutumia fursa ya Reli ya Mwendokasi na uwekezaji.

Kuhusu upelekaji wa fedha za Elimu Msingi na Sekondari zenye mazingira magumu na watoto wenye ulemavu.

Aliagiza na kusisitiza Halmashauri kuendelea kupeleka fedha kwenye Shule zenye mazingira magumu na zenye watoto Walemavu za Msingi na Sekondari kama vile Kilakala, Bungo, Mlimani, Mungi, Towero, Luhungo, Bigwa, Mkundi na Mbete.

Kuhusu upelekaji Shule watoto waliofaulu mitihani ya darasa la saba mwaka 2020.

Alisisitiza watoto wote waliohitimu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 wapelekwe shule walizopangiwa.

4.0 Salamu za Mkuu wa Wilaya ya Morogoro

Alieleza kuwa Wananchi wa Manispaa ya Morogoro wanamatumaini makubwa na Baraza la Madiwani hivyo aliwasihi Waheshimiwa Madiwani kuendelea kuwahudumia Wananchi.

Alieleza kuwa zipo changamoto chache zinazoikabili Halmashauri kuelekea kuwa Jiji hivyo aliagiza ziendelee kutatuliwa, Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa alishughulikia utatuzi wa changamoto ya Wafanyabiashara wa Soko Kuu la Chifu Kingalu zilizojitokeza wakati wa ziara ya aliekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati John Pombe Joseph Magufuli. Aliomba Madiwani na Watendaji kuendelea kushirikiana ili kuleta maendeleo.

Kuhusu elimu

Alisisitiza watoto wote waliofaulu mitihani ya kumaliza darasa la saba mwaka 2020 kujiunga na elimu ya Sekondari kwa shule walizopangiwa.

Kuhusu Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato

Alishauri Halmashauri ibuni vyanzo vipya vya mapato ili kuboresha maslahi na stahiki za Madiwani, Watumishi pamoja na Wananchi.

HMM/BM/31/2020/2021 Kuridhia Agenda za Mkutano

Baraza la Madiwani liliridhia agenda zifuatazo:-

1) Kufungua Mkutano.
2) Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.
3) Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 26/01/2021 (taarifa za Kata), tarehe 28/01/2021 (kawaida), na tarehe 10-11/03/2021 (Maalum - Bajeti).
4) Yatokanayo na mkutano maalum wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10—11/03/2021.
5) Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo:

5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 20/01/2021 (kawaida), tarehe 22/02/2021, tarehe 03/03/2021 na tarehe 18/03/2021.

5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya vikao vya tarehe 11/01/2021 (kawaida) na tarehe 23/02/2021.

5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira vikao vya tarehe 14/01/2021 (kawaida) na tarehe 26/02/2021 (Maalum – Bajeti).

5.4 Kamati ya kudhibiti UKIMWI vikao vya tarehe 15/01/2021 (kawaida) na 26/02/2021.

5.5 Kamati ya Maadili ya Madiwani kikao cha kawaida cha tarehe 23/04/2021.

6) Taarifa ya masuala ya kiutumishi.

7) Kufunga Mkutano.

HMM/BM/32/2020/2021
Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro

1.0 Kuhusu ukosefu wa Barabara Mtaa wa Fungafunga Kata ya Kichangani kuelekea Kata ya Mjimpya.

Swali

Mjumbe mmoja aliuliza kuwa ni lini Menejimenti itatatua changamoto ya ukosefu wa barabara Mtaa wa Fungafunga Kata ya Kichangani kuelekea Kata ya Mji Mpya.

Jibu

Ilielezwa kuwa changamoto ya ubovu wa Barabara lipo kwenye Kata nyingi, Halmashauri kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga fedha za kununua greda la Halmashauri. Hata hivyo kwa sasa matengenezo ya barabara yanafanywa na TARURA hivyo changamoto hiyo itapelekwa kwenye mamlaka hiyo kufanyiwa kazi.

2.0 Kuhusu mgogoro wa mipaka kati ya Chuo cha Ualimu Kigurunyembe na Wananchi wa Kata ya Kilakala

Mjumbe mmoja alieleza kuwa kuna mgogoro wa zaidi ya miaka 36 kati ya Chuo cha Ualimu Kigurunyembe na Wananchi wa Kata ya Kilakala, hivyo alitaka kujua ni nini utatatuliwa.

Jibu

Ilielezwa kuwa uthamini ulifanyika na taarifa ilipelekwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kulipa fidia lakini ilikataliwa na ilirudishwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Kwa sasa mgogoro huo unashughulikiwa na Ofisi ya Ardhi Mkoa.

3.0 Kuhusu kulipangia matumizi eneo la Manzese Pombe shop (lilipokuwa soko la muda)

Mjumbe alitaka kujua eneo la Manzese Pombeshop (lilipokuwa Soko la muda) Halmashauri ina mpango gani wa kulipangia matumizi baada ya Wafanyabiashara kurudi Soko Kuu la Chifu Kingalu.

Mjumbe alipendekeza Wafanyabiashara wa matunda kutoka Soko la Mawenzi na Fire wahamishiwe eneo hilo badala ya kuwapeleka Soko la Nanenane kwa kuwa wana mikopo wasije kushindwa kuirejesha. Pia eneo la Manzese kwa sasa lina vichaka hivyo lisafishwe.

Jibu

i) Ilielezwa kuwa kwa sasa mpango wa Halmashauri ni kuliimarisha Soko Kuu la Chifu Kingalu ndipo mpango wa kulipangia matumizi eneo la Manzese Pombeshop ufanyike.

ii) **Kuhusu Wafanyabiashara wa matunda Soko la Mawenzi**

Bado suala hilo linaendelea kufanyiwa kazi mahala pa kuwahamishia.

iii) **Kuhusu Wafanyabiashara waliopo Fire.**

Ilielezwa kuwa hao ni Wafanyabiashara ndogondogo waliokuwa wakifanyia biashara Mtaa wa Islam walipelekwa Fire kwa muda kwa kuwa biashara zao zina mitaji midogo na utaratibu mwingine unaendelea wa kuwatafutia eneo la kudumu.

iv) **Kuhusu usafi eneo la Manzese.**

Menejimenti imelichukuwa na kuahidi kulifanyia kaz.i

4.0 Kuhusu mradi wa upimaji viwanja eneo la Star City

Mjumbe mmoja alitaka kujua mradi wa upimaji viwanja kwenye eneo la shamba la Mkonge (Kilimanjaro Sisal Estate) umefikia wapi?

Jibu

Ilielezwa kuwa mradi wa Star City walipewa fedha za kulipa fidia Billioni 3 haikutekelezwa. Suala hili lipo kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hatua zaidi.

5.0 Kuhusu hali ya utoaji huduma kwenye Kitengo cha Biashara Manispaa

Ilielezwa kuwa Kitengo cha Biashara Manispaa ya Morogoro kinakabiliwa na msongamano mkubwa wa wateja wanaoenda kupata huduma hali inayopelekea ucheleweshwaji wa utoaji wa leseni za biashara hali inayotafsiriwa utoaji na upokeaji wa rushwa. Mjumbe alitaka kujua hatua za kutatua changamoto hiyo.

Jibu

Menejimenti ilifafanua kuwa Kitengo cha Biashara kitahamishiwa katika Stendi ya Daladala ya Mafiga pia zitakuwepo na ofisi nyingine kama vile Benki utalii hivyo huduma zote kufanyika kwenye kituo kimoja (one stop centre) hivyo kuondoa msongamano.

6.0 Kuhusu Watumishi kukaimu kwa zaidi ya miaka 6

Mjumbe alipendekeza Watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu wathibitishwe nafasi hiyo.

Jibu

Menejimenti iifafanua kuwa suala la Watumishi kukaimu kwa muda mrefu lilishafanyiwa kazi na kuwasilishwa kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuwaombea kibali wawe Wakuu wa Idara. Menejimenti inasubiri majibu.

HMM/BM/33/2020/2021 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 26/01/2021 (taarifa za Kata), tarehe

Mihtasari haikuwa na masahihisho hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za Mikutano.

28/01/2021 (kawaida), na tarehe 10-11/03/2021 (Maalum - Bajeti).

HMM/BM/34/2020/2021 Yatokanayo na mkutano maalum wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10—11/03/2021

Taarifa ya yatokanayo iliwasilishwa, ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

1.0 Kuhusu maeneo ya wazi na viwanja vya michezo

Azimio

Menejimenti iandae taarifa ya viwanja vya michezo na maeneo ya wazi na yaingizwe kwenye ziara ya robo ya tatu kwenye Kamati ya Mipangomij na Mazingira.

Utekelezaji

Agizo limezingatiwa. Timu ya Wataalam imeendelea kufanya uhakiki wa maeneo ya wazi. Taarifa ikikamilika itawasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.

Agizo

Baraza lilitoa muda wa mwezi mmoja kuanzia tarehe 29/04/2021 kazi ya kuhakiki maeneo ya viwanja vya wazi ikamlike na kuwasilisha taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.

2.0 Kuhusu ukodishaji wa uwanja wa Golf Course

Azimio

Baraza liliagiza Kamati ya Fedha na Uongozi kushughulikia suala la kuongeza kodi kwenye kitega uchumi cha Golf Course kwa kuwa kiwango kinacholipwa sasa cha **Tshs. 1,000,000.00** kwa mwezi ni kidogo.

Utekelezaji

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilishaingia mkataba katika kitega uchumi hiki kwa kodi ya **Tshs. 1,000,000.00** kwa mwezi kuanzia tarehe 01/07/2020 hadi tarehe 30/06/2021. Baada ya hapo Halmashauri itamwita na kukaa kuona namna bora ya kuongeza kiasi cha pango kwa mwekezaji.

3.0 Kuhusu kukatia bima miradi mikubwa ya Manispaa

Azimio

Baraza liliiagiza Kamati ya Fedha na Uongozi kukatia BIMA miradi mikubwa yote ya Halmashauri (Soko Kuu la Chifu Kingalu, Stendi ya Msamvu, DDC).

Utekelezaji

Utekelezaji umefanyika gharama za awali za kukatia bima Soko Kuu la Chifu Kingalu **0.35%** ni **Tshs. 57,000,000.00** kwa mwaka pamoja na (VAT) na Kitega Uchumi cha DDC **(0.15%)** ni **Tshs. 1,097,400** kwa mwaka pamoja VAT. Gharama hizo zinahusisha jengo pekee. Kuhusu Bima ya Stendi Kuu ya Msamvu utaratibu utafanyika baada ya makabidhiano ya Stendi hiyo kukamilika.

HMM/BM/35/ 2020/2021 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo

1.0 Kamati ya Fedha na Uongozi

Taarifa iliwasilishwa na ilipokelewa.

Mjadala na maamuzi

Kuhusu Kitega Uchumi cha DDC

Mjumbe mmoja alitaka kujua ni lini ujenzi wa Kitega Uchumi cha DDC utakamilika.

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa ujenzi utakamilika tarehe 15/05/2021. Baraza lilielekeza kuwa ujenzi ukikamilika na makabidhiano kufanyika fremu zitangazwe kwa uwazi, viongozi wa Halmashauri (Madiwani na Watendaji walitahadharishwa wasiombe ili wawaachie Wananchi wa kawaida kusudi yasije kutokea kama Soko Kuu la Chifu Kingalu.

Kuhusu usajili wa Vikundi vya mkopo ya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu

Mjumbe mmoja alitaka kujua mwitikio wa usajili wa vikundi vya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na anaehusika katika usajili na gharama.

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa anaehusika katika usajili ni Mkurugenzi wa Manispaa na gharama za usajili ni **Tshs. 50,000.00** hulipwa kupitia Benki.
Wajumbe walijulishwa kuwa Menejimenti imeandaa mafunzo ya Madiwani wote kuhusu kuwapa elimu ya suala hilo.

Kuhusu utaratibu wa kutangaza zabuni mbalimbali za Manispaa.

Baraza lilielekeza kuwa Menejimenti inapotangaza zabuni mbalimbali pia ilitoe tangazo kwenye gazeti la Serikali la Kiswahili linalosomwa na Wananchi wengi.

Kuhusu taarifa ya mgogoro wa shamba la Kilimanjaro Sisal Estate (Magereza Kihonda)

Mjumbe mmoja alitaka kujua mmiliki halali wa shamba la Kilimanjaro Sisal Estate na kama ujenzi unaofanyika una kibali cha ujenzi.

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa ujenzi unaoendelea eneo hilo unaofanywa na Jeshi la Magereza Kihonda hauna kibali cha ujenzi na walishapewa ilani ya zuio. Aidha suala la umiliki lilifikishwa kwa Makatibu Wakuu wa Wizara ya OR_ TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa sasa ujenzi umesimamishwa mpaka maamuzi ya nani mmiliki halali yatakapofanyika na Wizara.

Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa Waheshimiwa Madiwani wanapotaka kufanya ziara maeneo ya Jeshi iwe inatoa taarifa ili kuepusha migogoro.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya aliahidi kuuchukua mgogoro huo kuufuatilia kupitia vikao vya Kamati ya Chama.

Kuhusu uhaba wa Madawati katika Shule za Msingi na Sekondari.

Viongozi wa Kata ambao zina changamoto ya ukosefu wa madawati ya shule za Msingi na Sekondari waliagizwa wawasilishe maombi kwenye Kamati ya Mfuko wa maendeleo ya Jimbo.

Kuhusu ukataji wa mitiki kwenye Kata ya Boma na Kilakala

Baraza lilijulishwa kuwa ukataji wa mitiki kwenye Kata ya Boma na Kilakala kwa ajili ya kutengeneza madawati utaanza siku ya Jumatatu tarehe 03/05/2021.

Kuhusu uboreshaji wa maegesho ya magari eneo la Ofisi Kuu Manispaa

Wajumbe walitaka kujua Mkandarasi alitakiwa akabidhi kazi lini.

Ufafanuzi
Ilielezwa kuwa Mkandarasi alitakiwa akabidhi kazi tarehe 09/04/2021, Menejimenti imeanza kumkata fedha za kucheleweshe kazi kwa mujibu wa mkataba.

2.0 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya
Taarifa iliwasilishwa na ilipokelewa.

Kuhusu utendaji kazi wa Kampuni ya usafi wa Mazingira ya Kajenjere
Wananchi walisisitizwa kulipa ada ya uzoaji taka kwa wakati kwa Kampuni ya Kajenjere na Vikundi kazi ili kuleta ufanisi wa kazi. Aidha, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa waliagizwa kusimamia suala hilo.

3.0 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira
Taarifa iliwasilishwa ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

4.0 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

5.0 Maadili ya Waheshimiwa Madiwani
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

HMM/BM/36/2020/2021 Taarifa ya masuala ya kiutumishi

A: Mashauri ya nidhamu kwa Watumishi kumi (10) wa Kada mbalimbali:-

1. **Edson Othiniel Mukande (Msanifu Majengo Daraja II) Mashtaka yanayomkabili**:-
Utoro kuanzia tarehe 1/9/2019

Maamuzi ya Baraza la Madiwani
Afukuzwe kazi kwa kosa alilotenda

2. **Mwalimu Jane R. Shoo (Afisa Elimu Kata ya Uwanja wa Taifa)**
Mashtaka yanayomkabili
Kutokuwa muadilifu kwa mwajiri wake kwa kutumia pikipiki ya Halmashauri kwa shughuli zake binafsi za shamba katika kijiji cha Mvumi.
Maamuzi ya Baraza
Akatwe asilimia 15 ya mshahara wake kwa muda wa miaka mitatu.

3. **Elineema John Lyanga(Mteknolojia Msaidizi Maabara Kituo cha Afya Kingolwira)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro tangu amalize chuo mwaka 2019 hajaripoti kwenye Kituo chake cha kazi.

   Maamuzi ya Baraza
   Afukuzwe kazi kwa kosa alilotenda.

4. **Emanuel Ngowi (Tabibu wa meno katika kituo cha Afya Sabasaba)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro kazini kwa zaidi ya miezi miwili.

   Maamuzi ya Baraza
   Afukuzwe kazi kwa kosa alillotenda.

5. **Maria Z. Gerald (Muuguzi II Zahanati ya Madaganya)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro zaidi ya siku 5.

   Maamuzi ya Baraza
   Afukuzwe kazi kwa kosa alilotenda.

6. **Ever Leonard Bernard (Mhudumu wa Afya Mwandamizi Zahanati ya Kihonda)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro wa zaidi ya siku 5 kuanzia tarehe 1/5/2021.

   Maamuzi ya Baraza
   Afukuzwe kazi kwa kosa alilotenda.

7. **Johaness W. Bhoke (Tabibu I Kituo cha Afya Kingolwira)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro kuanzia tarehe 31/8/2020

   Maamuzi ya Baraza
   Afukuzwe kazi kwa makosa aliyotenda.

8. **Derick E. Runyoro (Muuguzi Kituo cha Afya Mafiga)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Utoro wa rejareja wa siku nne (4)

   Maamuzi ya Baraza
   Apewe onyo la maandishi kwa kosa alilotenda.

9. **Aikande Ndesaje Massawe (Afisa Afya Mazingira Msaidizi Mkuu)**
   Mashtaka yanayomkabili
   Kati ya tarehe 15/09/2020 hadi 11/02/2021 alitenda kosa la kutumia kizimba/kikazi ambacho ni mali ya Serikali alichokabidhiwa na Manispaa ya Morogoro na kumkodisha mtu mwingine Mwananchi na kumtoza gharama za juu zaidi kuliko gharama zilizowekwa na Manispaa.

   Maamuzi ya Baraza
   Kwa kuwa alimrudishia fedha Mwananchi alizochukuwa kumkodishia kizimba kwa gharama ya juu, Baraza la Madiwani lilimsamehe makosa aliyotenda aendelee na majukumu yake.

10. **Godfrey Joseph Maumba (Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kichangani kuanzia tarehe 25/7/2019 hadi 22/3/2020)**
    Mashtaka yanayomkabili
    Kufanya matumizi ya fedha **Tshs. 2,700,000.00** zilizokuwa kwenye Akaunti ya Kata ya Kichangani bila kufuata utaratibu na kusababisha upotevu wa fedha kiasi cha **Tshs. 2,700,000.00** (Milioni mbili Laki saba elfu) zilizokuwa kwenye akaunti ya Kata, hili ni kosa kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni ya 42, sehemu ya A jedwali la kwanza na Kanuni ya 13.

    Maamuzi ya Baraza
    Akatwe asilimia 15 ya mshahara wake kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu (3).

A. Taarifa ya Bodi ya Ajira kuthibitisha watumishi kazini

Ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma 2003, Kanuni ya 127, kila Halmashauri itaunda Bodi ya Ajira ambayo itashughulikia Mashtaka yote ya Ajira za Watumishi. Pia kwa mujibu wa Kanuni Na. 14 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 zikisomwa pamoja na Kanuni za kudumu za Utumishi wa

Umma za mwaka 2009 Kanuni D. 45 (1- 3), Mtumishi wa anayeajiriwa kwa mara ya kwanza katika Utumishi wa Umma atathibitishwa kazini baada ya kutumikia kipindi cha matazamio (probation period) kulingana na Muundo wa Utumishi wa Kada husika (Scheme of Service) kwa muda usiozidi kipindi cha miezi kumi na mbili (12) tangu tarehe ya kuajiriwa.

Kwa ufafanuzi huo Menejmenti iliwasilisha orodha ya Majina kama ifuatavyo:-

NA	JINA LA KWANZA	CHECK NA	CHEO CHA SASA	TAREHE YA AJIRA	KIWANGO CHA MSHAHARA
1	John Katungutu Joseph	112162775	Mtendaji wa Kata II	25-02-2019	TGS D1
2	Prisca Motera Richard	112245914	Mtendaji wa Kata II	01-09-2019	TGS D2
3	Cosmas Japhet Buhanga	112258830	Dereva II	02-12-2019	TGS B1
4	Daniel Hance Balence	112258837	Dereva II	02-12-2019	TGS B1
5	Azizi Rajabu Machela	112258846	Dereva II	02-12-2019	TGS B1
6	Benedictor Mgoso Gwambasa	112258862	Dereva II	02-12-2019	TGS B1
7	Edgar Anthony Mwakilasi	112272425	Dereva II	23-01-2020	TGS B1
8	Edson Othiniel Mnkande	112249885	Mkadiriaji Majenzi	01-10-2019	TGS E1

Maoni ya Menejimenti, Bodi ya Ajira na Kamati ya Fedha na Uongozi

Watumishi saba waliotajwa hapo juu wathibitishwe kazini na Mtumishi mmoja Ndg Edson Othiniel Mnkande – Mkadiriaji Majenzi asithibitishwe kwa kuwa ni mtoro hayupo kwenye kituo chake cha kazi na anashauri la kinidhamu.

Maamuzi ya Baraza

Baraza liliridhia Watumishi 7 wathibitishwe kazi kama ilivyooneshwa kuanzia Na 1-7 hapo juu na mtumishi mmoja Ndg Edson Othiniel Mnkande Mkadiriaji Majenzi asithibitishwe kazini kwa kuwa ana shauri la kinidhamu.

HMM/BM/37/ 2020/2021 Kufunga Mkutano

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa kuchangia hoja mbalimbali na maamuzi waliyoyafanya. Alimpongeza Mkurugenzi wa Manispaa na Wataalamu kwa kupeleka fedha kwenye Kata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Alisisitiza ukusanyaji wa mapato zaidi ili kupeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo kwenye Kata ili kumalizia miradi iliyokwishaanzishwa. Alifunga Mkutano saa 8:17 Mchana.

Muhtasari umethibitishwa tarehe .....

.....	.....
Mhe. Pascal M. Kihanga	Ndg. Sheilla E. Lukuba
MSTAHIKI MEYA	MKURUGENZI WA MANISPAA
MWENYEKITI	**KATIBU**

YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 29/04/2021

MUHT. NA	AZIMIO	MTEKELEZAJI	UTEKELEZAJI
HMM/BM/34/2020/2021 Yatokanayo na mkutano maalum wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10—11/03/2021	**4.0 Kuhusu maeneo ya wazi na viwanja vya michezo** Baraza lilitoa muda wa mwezi mmoja kuanzia tarehe 29/04/2021 kazi ya kuhakiki maeneo ya viwanja vya wazi ikamlike na kuwasilisha taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.	Afisa Mipangomiji na Maliasili wa Manispaa	Agizo limezingatiwa taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Mipangomiji na Mazingira